# KIZIDUO

## HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA.

MHUTASARI WA KIKAO CHA KAWAIDA CHA BODI YA ZABUNI CHA TAREHE 13/10/2021 KILICHOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA HALMASHAURI.

**WALIOHUDHURIA**

| JINA | CHEO |
|---|---|
| 1.SITTA SINGIBALA | MWENYEKITI |
| 2. MVANO A. KARUMBETE | KATIBU |
| 3.PATRICK MUHERE | MWANASHERIA |
| 4. ALTO MBIKIYE | MJUMBE |
| 5. BENSON P. MIHAYO | MJUMBE |
| 6.NEEMA SEMWAIKO | MJUMBE |

**WASIOHUDHURIA**

| | |
|---|---|
| 1.SHUKRAN KYANDO | KWA TAARIFA |

**WAALIKWA**

| | |
|---|---|
| 1. PETRO YOHANA | AFISA USAFISHAJI |

**SECRETARIETI**

| | |
|---|---|
| 1. MARIANA MGOMI | AFISA UGAVI |

**AGENDA**

1. KUFUNGUA KIKAO
2. KURIDHIA AGENDA
3. KUSOMA NA KUIDHINISHA MIHTASARI YA TAREHE 19/06/2021 NA 29/06/2021.
4. YATOKANAYO NA MUHTASARI WA TAREHE 19/06/2021 NA 29/06/2021
5. KUSUDIO LA KUVUNJA MKATABA NA: - LGA/159/2020/2021/NC/08 - II – USOMBAJI WA TAKA NGUMU KANDA A – INAYOHUSISHA KATA ZA ILEMELA, KISEKE, KIRUMBA, IBUNGILO, PASIANSI, NYAMANORO, KITANGIRI, NA KAWEKAMO
6. OMBI LA KUTEKELEZA UJENZI WA KITUO CHA AFYA CHA KAYENZE KWA NJIA YA FORCE ACCOUNT.
7. OMBI LA UNUNUZI WA LORRY TANI 7 KWA NJIA YA NUKUU YA BEI (COMPETITIVE QUOTATION).

CamScanner

8. OMBI LA UNUNUZI WA PIKIPIKI 14 KWA AJILI YA MAAFISA UGANI NA 12 KWA AJILI YA WATENDAJI WA KATA.
9. TAARIFA YA MUONGOZO WA UTEKELEZAJI WA MIRADI KWA NJIA YA SINGLE SOURCE.
10. TAARIFA YA MANUNUZI YALIYOFANYIKA KWA NJIA YA CIRCULAR RESOLUTION.
11. KUPOKEA NA KUIDHINISHA TAARIFA YA TATHIMINI UFUNGUAJI NA UJENZI WA BARABARA MPYA KATIKA MRADI WA VIWANJA WA EAST BUSWELU.
12. KUFUNGA KIKAO.

**MUHT/TB/NA.09/2021/2022 – TAARIFA YA MUONGOZO WA UTEKELEZAJI WA MIRADI KWA NJIA YA SINGLE SOURCE. (UJENZI WA MADARASA YA SEKONDARI 97 YA UVIKO-19.**

Kwa Mamlaka iliyopewa Mamlaka ya Kuthibiti Ununuzi wa Umma (PPRA), kifungu cha 9 (c) cha sheria ya sheria ya Manunuzi Na 7 ya 2011, imetoa Muongozo wa tarehe 12/10/2021, wenye kumb Na CA.192/211/01/74, ukizitaka Taasisi Nunuzi zote kutekeleza kazi kwa kuzingatia njia ya Single Source, kwa lengo la kuhakikisha Miradi inakamilika kwa Wakati.

Aidha utaratibu wa Single Source umeelezwa kwenye kanuni ya 159, 160 na 161 ya kanuni za manunuzi ya umma GN446 ya 2013, iliyofanyiwa marekebisho GN 333 ya 2016.

Hivyo kwa kutumia njia hii, Mchakato wa Kumpata Mkandarasi unaweza kukamilika ndani ya siku moja, kwani haina muda maalumu wa Utekelezaji (rejea jedwali la 8), isipokuwa inahitaji Mkandarasi/Mzabuni kupewa Nukuu ya bei, baada ya kuwasilisha bei yake yanafanyika majadiliano na kisha Mkataba wa kazi unasainiwa.

Katika njia hii inahitaji Mkandarasi/Mzabuni awe na uwezo (kifedha na mitambo), uzoefu na wafanyakazi wa kutosha, ili kuweza kazi kukamilika kwa wakati.

MAPENDEKEZO YA PMU

PMU inapendekeza kwa Bodi ya zabuni kwamba kwa kuzingatia muongozo huo, basi miradi inayofuata tukianza madarasa 97 ya sekondari yalitangazwa kupitia Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO – 19, yatekezwe kwa kuzingatia muongozo huu.

UAMUZI WA BODI YA ZABUNI

Bodi ya zabuni mara baada ya kupokea taarifa hiyo waliridhia Mapendekezo ya PMU na kuridhia miradi itekelezwe kwa njia ya Single Source kuanzia mradi wa Madarasa ya Sekondari 97.

CamScanner

Baada ya uamuzi huo, Bodi ya zabuni ilitaka kufahamu kwamba ni Shule zipi ambazo zimekusudiwa katika ukamilishaji wa Madarasa hayo 97. Katibu alijibu kwamba taarifa ya shule hizo hana, hivyo Wajumbe waliagiza Afisa Elimu Sekondari aitwe kwa ajili ya kutoa ufafanuzi. Baada ya Afisa Elimu Sekondari (Ndg Emmanuel Malima) kufika , alitoa ufafanunuzi kama ifuatavyo:- "Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela imepokea jumla ya Tshs 1,940,000,000.00) kwa ajili ya ujenzi wa vyumba 97 vya madarasa na viti na meza 50 kwa kila darasa, kwa uzingatio wa kiti 1 na Meza 1 kwa Mwanafunzi 1 na kila darasa linatarajiwa kugharimu kiasi cha Tshs 20,000,000.00 ikijumwisha Ujenzi wa darasa pamoja na Viti na Meza".

Baada ya maelezo hayo Afisa Elimu alitaja mgawanyo wa Vyumba 97 kama ifuatavyo:- Bugogwa Sekondari vyumba 5, Kisundi Sekondari Vyumba 5, Bujingwa Sekondari Vyumba 4, Buswelu Sekondari vyumba 5, Ibungilo Sekondari vyumba 4, Kiloleli Sekondari vyumba 5, Lumala Sekondari vyumba 6, Lukobe Sekondari vyumba 2, Kilimani Sekondari vyumba 2, Pasiansi Sekondari vyumba 3, Kayenze Sekondari vyumba 6, Kabuhoro Sekondari vyumba 2, Kirumba Sekondari vyumba 3, Mihama Sekondari vyumba 2, Mwinuko Sekondari vyumba 2, Nundu Sekondari vyumba 5, Kangaye Sekondari vyumba 4, Nyamanoro Sekondari vyumba 2, Ibinza Sekondari vyumba 3, Nyasaka Sekondari vyumba 6, Bwiru Boys Technical Sekondari vyumba 5, Kitangiri Sekondari vyumba 2, Mnarani Sekondari vyumba 2, Sangabuye Sekondari chumba 1, Shibula Sekondari vyumba 6, na Angeline Mabula Sekondari vyumba 5.

Wajumbe mara baada ya kupokea taarifa hiyo waliiridhia na kisha kumuagiza Afisa Elimu ahakikishe kazi hizo zinakamilika mapema kama ilivyoagizwa.

**MUHT/TB/NA. 12/2021/2022 - KUFUNGA KIKAO**

Mwenyekiti alifunga kikao mnamo saa 08.49 mchana kwa kuwashukuru wajumbe wote kwa ushirikiano walitoa.

| MWENYEKITI | KATIBU |
|---|---|
| JINA...Sitta Singibala... | JINA.../Limi P. George... |
| SAHIHI...[signature]... | SAHIHI...[signature]... |

TAREHE YA KUTHIBITISHWA MHUTASARI...13/01/2022.

CamScanner